Jina…… **Nambari Yako……**

Sahihi…….. **Tarehe……**

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
JULAI/AGOSTI 2010
MUDA: SAA 2 ½

TATHMINI YA PAMOJA YA WILAYA ZA BORABU-MASABA – 2010

Kenya Certificate of Secondary Education – (KCSE)

KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
JULAI/AGOSTI 2010
MUDA: SAA 2 ½

MAAGIZO

- Andika jina na nambari yako hapo juu.
- Weka sahihi na tarehe.
- Jibu maswali yote.
- Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki.
- Hakikisha kuwa kurasa zote zimechapishwa.

Swali	**Upeo**	**Alama**
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa.
Mtahiniwa ahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sana sana na kuwa maswali yote yamo.

1. Ufahamu (alama 15)

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali:

Mjumbe huyu aliishauri Kusadikika kama iliweza kufikiri kutengeneza tayari bandari na viwanja vya kutua vyombo hivyo. Kwa shauri hili, alidhihakiwa kuwa alikuwa kama mama aliyekuwa akimwandalia mtoto aliyekuwa bado kuzaliwa. Ilisadikika kuwa watu wa Ardhi walikuwa hawawezi kuvumbua njia ya kuunda vyombo vya kusafiri hewani hata kama waliweza kusafiri baharini na barani. Kwa hivi, Kusadikika ilikuwa haina haja ya kutengeneza tayari bandari wala viwanja kwa ajili ya vyombo vya Ardhi. Andao lolote kwa ajili ya wakati ujao lilikuwa upuzi kwa washauri wa Kusadikika.

Amini aliwaonya kuwa kama wakati ujao hauandaliwi mbele vema, hasara zake zitakuwa kubwa. Lakini walishikilia kusema kuwa maharibiko ya wakati huo yalikuwa si juu yao, ingawa walijua barabara kuwa watu watakaoishi katika wakati huo ni watoto wao wenyewe. Shauri hili lilikuwa si upuzi. Lilikuwa ni shauri la hekima sana.

Udhahiri wa mambo ni kuwa ulimwengu uliumbwa kabla ya wakaaji wake. Kama ulimwengu usingalitangulia kuumbwa, wakaaji wake wasingalikuwa na mahali pa kukaa. Ukitaka biashara ya vitabu istawi watu hawana budi kufunzwa kusoma kwanza. Kusoma kusipotangulia, vitabu vizuri vitaonekana vibaya. Kabla ya kujenga msikiti, watu lazima wafunzwe utukufu wa dini mbele. Bila ya hivyo msikiti mtukufu utakuwa kama mkahawa mchafu tu. Kadhalika mfano, kama nchi haina bandari ya namna yoyote, haiwezi kutazamia kufikiwa na vyombo. Kila azimio katika maisha hutaka neno fulani kufanyizwa mbele ili kuyashawishi maendeleo yake. Watu watakao kustawi katika maisha huelekeza bidii zao juu ya mshawasha wa makusudi yao kwanza. Kama hili si shabaha ya kwanza katika maisha, basi, haiwi ya pili kwa nyingine yoyote. Mambo yaliyo makubwa na madogo yamefungamana na utaratibu huu.

Maswali:

a) Kwa kutoa sababu, Kusadikika ilikuwa katika hali gani kimaendeleo. (alama 2)

……

……

……

……

b) Je, ni vema mama kumwandalia mtoto ambaye hajazaliwa? Tetea jibu lako. (alama 2)

……

……

……

……

c) Andika hoja alizozitoa mwandishi dhidi ya busara ya methali: “Usikate kanzu kabla mtoto hajazaliwa”. (alama3)

……

……

……

……

……

……

d) Wakati ujao usipoandaliwa vema, hasara zake zitakuwa gani kwa kurejelea taarifa? (alama 2)

……

……

……

……

e) Kutokana na habari hii, ni kwa nini nchi ya Kusadikika haikufikiwa na wajumbe kutoka nchi nyingine? (alama 2)

……

……

……

……

f) “Watu watakao kustawi katika maisha huelekeza bidii zao juu ya mshawasha wa makusudi yao kwanza”. Fafanua. (alama 2)

……

……

……

……

g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa kifunguni. (alama 2)

i) Kutazamia

……

……

ii) Mshawasha

……

……

2. Ufupisho (alama 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:

Kila jambo tufanyalo kuhusiana na lugha husitawisha ufahamu wetu wa mambo tusomayo. Mazoezi katika kuandika husitawisha ufahamu katika kusoma kwa sababu katika kuandika ni lazima tujaribu kuyatumia maneno vizuri na kufahamu ugumu wa usemi. Twajifunza matumizi ya kugha katika kuzungumza na kuwasikiliza wengine wakizungumza. Lugha tusomayo ikiwa imeandikwa hasa huwa ni aina ya lugha ya mazungumzo vile vile. Kuna ujuzi mwingi katika kuzungumza upatikanao katika shule – kama vile michezo ya kuigiza, hotuba, majadiliano na mazungumzo katika darasa na haya yote husaidia katika uhodari wa matumizi ya lugha.

Ujuzi wa kila siku hutasaidia katika maendeleo ya kusoma na usitawi wa msamiati. Ikiwa mwanafunzi amemwona ndovu hasa, atakuwa amejua maana ya neno ndovu vizuri zaidi kuliko mwanafunzi ambaye hajapata kumwona ndovu bali ameelezwa tu vile alivyo. Vile vile ujuzi wa kujionea sinema au michoro husaidia sana katika kusoma. Kwa hivyo kwa njia fulani mambo yote juu ya ujuzi wa kila siku husaidia kufahamu mambo yaliyoandikwa. Ikiwa mwanafunzi ana huzuni au ana furaha, akiwa mgonjwa au amechoka au amesifiwa, haya yote ni ujuzi. Wakati ujao mwanafunzi asomapo juu ya mtu ambaye amepatikana na mambo kama hayo hana budi kufahamu vizuri zaidi.

Karibu elimu yote ulimwenguni huwa imeandikwa vitabu lakini lugha zote hazina usitawi sawa kuhusu fasihi. Kwa bahati mbaya lugha nyingine hazijastawi sana na hazina vitabu vingi lakini katika lugha nyingine karibu mambo yote yanayohusiana na elimu huweza kupatikana katika vitabu. Inambidi mwanafunzi anayejifunza asome vitabu au majarida juu ya sayansi au siasa au historia, lakini haimbidi kusoma tu juu ya taaluma fulani anayojifunza. Inafaa asome juu ya michezo, mambo ya shani, na juu ya mahali pageni ili kupata ujuzi wa mambo mengi mbali mbali.

Maswali:

a) Fupisha aya za kwanza mbili kwa kutumia maneno 65. (alama 10, 2 za utiririko)

Maandalizi

……

……

……

……

……

……

……

……

……

Jibu:

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

b) Kwa kuzingatia habari zote muhimu na bila kupoteza maana asilia, fupisha aya ya mwisho. (Maneno 30, alama 5 , 1 ya utiririko).

Maandalizi:

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

Jibu:

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

3. Matumizi ya lugha (alama 40)

a) Eleza matumizi yoyote matatu ya kiimbo. (alama 3)

i) ……...

ii) ……..

iii) …….

b) Onyesha mfumo wa sauti katika tungo: Mtumbwini. ((alama 2)

……

……

……

……

c) Andika sentensi hizi kulingana na maagizo uliyopewa mabanoni. (alama 2)

i) Tulitoa kodi kubwa kwa serikali.

(Anza: Serikali……)

……

……

ii) Tano ondoa tatu ni mbili: (Anza: Mbili……)

……

……

d) Unda vitenzi viwili viwili kwa kila mojawapo ya maneno uliyopewa: (alama 2)

i) Uchafu

……

……

ii) Mkopo

……

……

e) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mishale. (alama 4)

Mama na baba wako mtini.

……

……

……

……

……

……

……

……

f) Ukizingatia nafsi tambua na uonyeshe aina za mofimu katika sentenzi hii: Sisi tunampenda yeye tu. (alama 2)

……

……

……

……

g) Toa matumizi yoyote matatu ya 'Na" (alama 3)

i) ……..

ii) ……..

iii) …….

h) Tunga sentensi moja ukitumia vitate vifuatavyo ili kuonyesha matumizi yao: (alama 2)

i) Ngoma

……

……

ii) Goma

……

……

i) Bainisha majukumu ya viambishi katika neno hili: Akuchezea. (alama 2)

……

……

……

……

j) Fundi mzuri ni aliyetualika kwake. (alama 2)

Onyesha kundi nomino na kundi tenzi.

……

……

……

……

k) Tofautisha: (alama 2)

i) Mwenye mali amefika.

……

……

ii) Mwenyewe anapendeza.

……

……

l) Tunga sentensi yenye kihusishi cha ‘a’ – unganifu katika ngeli ya U – ZI. (alama 2)

……

……

……

……

m) Mbwa wetu amekatwa mkia. Geuza katika hali ya ukubwa. (alama 2)

……

……

……

……

n) Sentensi hii iko katika hali gani? Kwamboka na mama wacheza uwanjani. (alama 2)

……

……

……

……

o) Nywele zao zilinyolewa zote. Andika kwa umoja. (alama 2)

……

……

……

……

p) Kanusha sentensi hizi: (alama 2)

i) Analia na kulaani.

……

……

ii) Akiniona nitamfurahisha.

……

……

q) Sahihisha. Ukikula sana utagonjeka. (alama 2)

……

……

……

……

r) Nyambua vitenzi hivi viwe katika kauli ya kutendana: (alama 2)

i) la

……

……

ii) lia

……

……

4. Isimu-jamii

Taja na kueleza njia zozote tano zinazochangia maenezi ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya.

(alama 10)

……

……

……